**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI ILIYOFANYIKA TAREHE 11 MACHI,2022 KATIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA.**

**MAHUDHURIO**

| NA. | JINA | CHEO |
|---|---|---|
| 1. | Abushiri Mbwana | Mwenyekiti wa bodi |
| 2. | Tunu Mtamah | Katibu wa bodi |
| 3. | Grace Mwambe | Mjumbe |
| 4. | Silvester Kalagila | Mjumbe |
| 5. | Juma J.Ahmad | Mjumbe |

**WAALIKWA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Eng.Said Pongwa | Mwalikwa |
| 2. | Peter Abillus | Mwalikwa |
| 3. | Dr.Mahela Njile | Mwalikwa |

**SEKRETARIET**

Abdalah Mchwembo

**MWANDISHI**

Julius Mayega

**Agenda.**

**1/2022.KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliwakaribisha wajumbe katika kikao nakuwaeleza kuwa hiki ni kikao cha kawaida cha bodi kujadili masuala mbalimbali ya manunuzi,baada ya hapo alimkaribisha mwenyekiti ili afungue kikao.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika kikao nakuwaeleza kuwa tuwe makini katika kujadili agenda zilizowasilishwa kikaoni kwa maslahi mapana ya Halmashauri,baada ya hapo alifungua kikao mnamo saa 2:20 asubuhi.

## 2/2022.KUTHIBITISHA AGENDA

Jumla ya agenda tisa(9) ziliwasilishwa kikaoni ambazo ni;

i. Kufungua kikao
ii. Kuthibitisha agenda
iii. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha bodi ya zabuni kilichofanyika tarehe 29 Novemba,2021
iv. Yatokanayo na kikao cha bodi ya zabuni ya kilichofanyika tarehe 29 Novemba,2021
v. Kupitia ripoti ya tathmini ya mtaalamu mshauri(CONSULTANT)wa athari za mambo ya mazingira miradi ya ujenzi wa stendi ya mabasi Nangurukuru,ujenzi wa jengo la utawala Lingaula,ujenzi wa soko la kisasa la samaki mji mdogo Kilwa Kivinje na ujenzi wa shule ya sekondari Ngome.
vi. Idhini ya kufanya ujenzi wa jengo la dharura katika hospitali ya Wilaya Kinyonga kwa gharama ya Tsh.300,000,000/= na nyumba ya mtumishi katika kituo cha Afya Hoteli Tatu wenye thamani ya Tsh.90,000,000/=
vii. Maombi ya matumizi ya fedha kiasi cha Tsh.21,140,000/=kwa ajili ya matengenezo ya barabara 2km ya kwenda shule ya sekondari Ngome na maandalizi ya ujenzi wa jengo la utawala Lingaula
viii. Idhini ya kufanya ujenzi wa jengo la wodi ya wazazi lenye chumba cha upasuaji, jengo la kufulia nguo na korido(walk way) katika kituo cha afya Hotel tatu kwa gharama ya shilingi 250,000,000/=
ix. Mengineyo kwa Idhini ya mwenyekiti
x. Kufunga kikao.

Wajumbe walipokea nakuridhia agenda hizo zijadiliwe katika kikao.

## 3/2022.KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI KILICHOFANYIKA TAREHE 29 NOVEMBA, 2021.

Muhtasari wa kikao cha bodi kilichofanyika tarehe 29 Novemba 2021 uliwasilishwa, Wajumbe waliupokea muhtasari huo,waliupitia ukurasa kwa ukurasa na ukawekwa saini na Mwenyekiti na Katibu kuwa kumbukumbu halali ya Halmashauri.

**4/2022.Yatokanayo na kikao cha bodi ya zabuni ya kilichofanyika tarehe 29 Novemba,2021.**

Yatokanayo na kikao cha bodi ya zabuni kilichofanyika tarehe 29 Novemba, 2021 yaliyowasilishwa,Wajumbe walitaka ufafanuzi kuhusu kulipwa posho za vikao vilivyopita.

Katibu alitoa ufafanuzi kuwa madokezo yalishapelekwa ofisi ya MwekaHazina na yameandikiwa na vifungu vya kufanya malipo hayo, aidha mpaka muda huu fedha hizo hazijatoka.

Wajumbe walipokea ufafanuzi huo nakusisitiza kuwa katibu aendelee kufuatilia malipo hayo kwa MwekaHazina.

**5/2022.**Kupitia ripoti ya tathmini ya mtaalamu mshauri(CONSULTANT)wa athari za mambo ya mazingira miradi ya ujenzi wa stendi ya mabasi Nangurukuru,ujenzi wa jengo la utawala Lingaula,ujenzi wa soko la kisasa la samaki Kilwa Kivinje na ujenzi wa shule ya sekondari Ngome.

Mhandisi wa ujenzi wilaya alieleza kuwa fedha za kutengeneza barabara kwenda shule ya sekondari Ngome zinatoka benki ya dunia(WB) tukaona tufanye tathmini haraka ili tusikwamishe mradi,pamoja na miradi mingine ya maji.

Afisa Mazingira alieleza kuwa katika miradi hii mikubwa ni lazima tathmini ya athari ya mazingira ifanyike, aidha aliyependekezwa ndiye atakayefanya tathmini hiyo kwa miradi yote mitatu na kila mradi tathmini yake itafanyika kwa gharama za Tsh.16,000,000/=

Wajumbe walikubaliana kwa pamoja kuwa waliopendekezwa kufanya tathmini ya athari ya mazingira katika miradi mitatu(3) wafanye kazi hizo.

**6/2022.**Idhini ya kufanya ujenzi wa jengo la dharura katika hospitali ya Wilaya Kinyonga kwa gharama ya Tsh.300,000,000/= na nyumba ya mtumishi katika kituo cha Afya Hoteli Tatu wenye thamani ya Tsh.90,000,000/=

Katibu alitoa ufafanuzi kuwa alipokea dokezo toka idara ya ujenzi kuhusu matumizi ya fedha kiasi cha Tsh.300,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa jengo la dharura hospitali ya wilaya Kinyonga na Tsh.90,000,00/= kwa ajili ya ujenzi wa  nyumba ya mtumishi.

Wajumbe walipokea walijadili na kuridhia maombi hayo,aidha walikubaliana kuwa ujenzi huo ufanyike kwa njia ya **FORCE ACCOUNT**.

**7/2022.**Maombi ya matumizi ya fedha kiasi cha Tsh.21,140,000/=kwa ajili ya matengenezo ya barabara 2km ya kwenda shule ya sekondari Ngome na maandalizi ya ujenzi wa jengo la utawala Lingaula.

Katibu alitoa ufafanuzi wa matumizi ya fedha kiasi cha Tsh. 21,140,000/=kwa ajili shughuli za  matengenezo ya barabara ya 2km ya kwenda shule ya Sekondari Ngome

na maandalizi ya ujenzi wa jengo la Utawala Lingaula. Aidha alitoa mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo kuwa kiasi cha Tsh.11,140,000/= zitatumika kwenye maandalizi ya ujenzi wa jengo la utawala Lingaula na fedha kiasi cha Tsh.10,000,000/= zitatumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya kilomita mbili(2) ya kwenda shule ya sekondari Ngome.

Afisa mipango alieleza kuwa fedha za shughuli hizi ilipaswa kutoka katika mapato ya ndani ya Halmashauri, ila kwa sasa Halmashauri haina fedha, tumekubaliana Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri kuwa tutumie fedha za mradi alafu zitarejeshwa baada ya Halmashauri kupata fedha.

Wajumbe walipokea maombi ya fedha kiasi cha Tsh.21,140,000/= pamoja na mchanganuo wake,aidha wajumbe walijadili suala hili kwa kina nakuridhia matumizi ya fedha hizo, pia walisisitiza fedha hizo zitumike kwa ajili shughuli ziliyopangwa na kazi hizo zisimamiwe kikamilifu kwa ajili ya manufaa ya Halmashauri kwa ujumla.

**8/2022.**Idhini ya kufanya ujenzi wa jengo la wodi ya wazazi lenye chumba cha upasuaji, jengo la kufulia nguo na korido(walk way) katika kituo cha afya Hotel tatu kwa gharama ya shilingi 250,000,000/=

Katibu alieleza kuwa alipokea maombi ya dokezo la ujenzi wa wodi ya wazazi lenye chumba cha upasuaji, jengo la kufulia nguo na korido(walk way) katika kituo cha afya Hotel tatu kwa gharama ya shilingi 250,000,000/=

Mganga Mkuu wa wilaya alieleza kuwa ujenzi wa jengo la wodi ya wazazi lenye chumba cha upasuaji, jengo la kufulia nguo na korido(walk way) katika kituo cha afya Hotel tatu unaendelea vizuri.

Wajumbe walipokea walijadili nakuridhia fedha zilizoombwa zitumike kwa kazi zilizopangwa.

**9/2022.MENGINEYO.**

Hakuna mengineyo yaliyowasilishwa.

**10/2022.KUFUNGA KIKAO**

Katibu aliwashukuru wajumbe kwa kujadili vizuri agenda zilizowasilishwa kikaoni,baada ya hapo alimkaribisha mwenyekiti ili afunge kikao.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa mahudhurio yao,pia alimsisitiza Katibu afuatilie posho za wajumbe kwa mwekahazina kwakuwa wajumbe wanadai karibu vikao vyote ambavyo vimekwisha kufanyika hapo awali. Alifunga kikao mnamo saa 9:30 asubuhi.

**Saini ya mwenyekiti**......................**Saini ya katibu**..............................

**Tarehe**....10/05/2022......................